

1. kufanya kazi yoyote ambayo inatakiwa ku tekelezwa na wakili tu.
 2. kutoza gharama yoyote ya kitaalam kwa ajili ya huduma ya msaada wa kisheria aliyoitoa kwa muhitaji.
- Mtu anayekiuka masharti haya anatenda kosa linalostahili adhabu ya faini isiyopungua shillingi 1,000,000/= au kifungo kisichozidi miezi mitatu, au vyote kwa pamoja.

3.0 HITIMISHO

Sheria ya Msaada wa Kisheria imeweka msingi wa utekelezaji wa haki ya kuwakilishwa kwa kuweka mfumo ambao unasaidia watu wasio na uwezo kupata huduma ya msaada wa kisheria kutoka vyombo vya kutoa misaada wakiwemo wasaidizi wa kisheria. Maboresho haya ni muhimu katika kuhakikisha upatikanji haki wa wote

Kwa Maoni, wasiliana na Tume kupitia anuani ifuatayo :

Katibu Mtendaji,
Tume ya kurekebisha Sheria
Tanzania ,

Jengo la Taaluma Na. 1,
Barabara ya Mkalama
S.L. P 1718
DODOMA
TANZANIA

Barua pepe: lrct@lrct.go.tz
Tovuti: www.lrct.go.tz

TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA



SHERIA YA MSAADA WA KISHERIA



1.0 UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Tume) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume. Kwa mujibu wa sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kufanya mapitio na kutathimini utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kitekinolojia.

Katika kutekeleza jukumu hili, mwaka 2004, Tume imefanya mapitio na kuandaa Taarifa kuhusu Mfumo wa kutoa Msaada wa Kisheira kupitia Wasaidizi wa Sheria. Miongoni mwa mapendekezo yaliyotolewa ni kutungwa kwa sheria mahsusii ya kusamamia utoaji wa msaada wa kisheria.

2.0 SHERIA YA MSAADA WA KISHERIA

Mwaka 2017 Sheria ya Msaada wa Kisheria ililitungwa. Sheria ina malengo ya kuwatambua wasaidizi wa kisheria na kuboresha utoaji wa msaada wa kisheria, Sheria imeanisha mambo yafuatayo:

2.1 Msajili wa Watoa Huduma za Sheria

Msajili wa watoa huduma za kisheria anateuliwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria kutoka miongoni mwa watumishi wa Wizara hiyo. Sheria inawatambua wasajili wasaidizi ambao ni maafisa wa kada ya jamii, wanaofanya kazi katika sekretariati ya

Mkoa, Wilaya, Halmashauri za Majiji, Manispaa, Mamlaka za Miji na Halmashauri za Wilaya.

2.2 Majukumu ya Msajili

Miongoni mwa majukumu ya Msajili ni:
Kusajili watoa huduma;
Kuchunguza malalamiko ya wananchi kuhusu makosa ya kimaadili ya watoa huduma;
Kutunza rejeta ya watoa huduma ya msaada wa kisheria.
Kufanya ukaguzi wa ofisi za watoa huduma ili kujiridhisha ubora wa huduma zitolewazo.

2.3 Sifa za Msaidizi wa Kisheria

Elimu ya Shahada ya fani yoyote kutoka taasisi inayotambuliwa, isipokuwa shahada ya sheria ;
Elimu ya Stashahada au astashahada (Cheti) katika fani yoyote kutoka taasisi yoyote inayotambuliwa; au
Cheti cha elimu ya sekondari.

2.4 Usajili

Msaidizi wa sheira anatakiwa kuomba kwa Msajili wa Huduma za Msaada wa Sheria kusajiliwa. Katika maombi hayo ataambatanisha nakala za vyeti vya shahada, stashahada au astashahada (cheti). Vile vile anatakiwa kuwa na:
1.Cheti kinachoonyesha uelewa wake katika Katika kutoa msaada wa kisheria :

- 2.uthibitisho kuhusu mwenendo wake kutoka kwa msimamizi wake;
 - 3.Uthibitisho kutoka kwa mtu ambaye amemuona muombaji akitoa msaada wa kisheria;
 - 4.Uthibitisho kuhusu mwenendo wake kutoka kwa kiongozi wa kitongoji wa eneo lake la kikazi; na malipo ya ada.
- Msajili anaweza kukataa maombi ya usajili ikiwa atajiridhisha kuwa maombaji:
- 1.Hajatimiza masharti yanayotakiwa;
 - 2.Amewasilisha taarifa za uongo au kilaghai

2.5 Wajibu wa Wasaidizi wa Sheria

Kwa mujibu wa sheria, wasaidizi wa sheria wana wajibu wa

- 1.kuendesha mafunzo kuhusu masuala ya sheria na taratibu;
- 2.Kumsaidia mteja kupata nyaraka muhimu za kisheria;
- 3.Kumueleza mteja njia sahihi ya kupata haki yake; na
- 4.Kushauri pande zote zinazopingana na kutafuta suluhu ya mgogoro au kuwaelekeza kwenye vyombo vinavyohusika na utatuzi wa migogoro

2.6 Makatazo

Katika kutoa msaada wa kisheria, Msaidizi wa sheria haruhusiwi kujihusisha na: